



PARLIAMENT  
OF KENYA  
LIBRARY



REPUBLIC OF KENYA

# Speech

by

His Excellency

Hon. Uhuru Kenyatta, C.G.H.

President and Commander-in-Chief of the Defence  
Forces of the Republic of Kenya

on the occasion of

**State Opening of the 1st Session**

at

Parliament Building

on

Tuesday, 16th August

**HOTUBA YA MHESHIMIWA UHURU KENYATTA,  
C.G.H., RAIS NA AMIRI JESHI MKUU WA VIKOSI VYA  
ULINZI VYA JAMHURI YA KENYA WAKATI WA  
UFUNGUZI RASMI WA BUNGE LA KUMI NA MOJA,  
JUMANNE, 16 APRILI, 2013**

MASPIKA WA SENETI NA BUNGE LA TAIFA,  
WAHESHIMIWA WABUNGE;

Ni heshima kuu kuhutubia kikao cha ufunguzi cha Mabunge haya mawili. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuchaguliwa na kuteuliwa katika Bunge la Seneti na Bunge la Kitaifa.

Vile vile, nawapongeza Spika wa Bunge la Kitaifa na Spika wa Bunge la Seneti pamoja na manaibu wao kufuatia kuchaguliwa kwao. Pia, nampongeza kiongozi wa serikali bungeni na kiongozi wa chama cha upinzani na manaibu wao kwa kuchaguliwa katika nyadhifa hizo. Hasa ninawapongeza wanawake wengi waliochaguliwa katika mabunge yote, hili likiwa ni dhahirisho la kujitolea kwa Kenya kuafikia usawa wa kijinsia. Nalipongeza bunge lililopita kwa kupitisha miswaada mingi na kutimiza muda uliowekwa kikatiba. Nawatakia Waheshimiwa Wabunge wote kila la kheri mnapoongoza ajenda ya kutunga sheria na maongozi ya bunge hili katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Sote tulishiriki katika utaratibu wa uchaguzi ambapo tulifanya kampeini katika kaunti na maeneo bunge mbali mbali; tukiwania viti mbali mbali na kukampeinia vyama na miungano tofauti tofauti. Leo hii, tuko hapa kwa kusudi moja la kuimarisha maslahi ya Wakenya, kulinda haki za Wakenya na kutoa sauti kwa maslahi ya Wakenya. Tuko hapa sio tu kwa ajili yetu bali kama waakilishi wa wananchi.

Leo hii, lazima tutambue kwamba tuko chini ya Katiba mpya. Katiba ambayo ilibuniwa na bunge na kuidhinishwa na Wakenya kama sheria kuu ya nchi. Tukiwa watungaji sheria,

jukumu letu la kwanza ni kutii sheria kulingana na Katiba. Nawahimiza sisi sote kukumbuka kwamba kila mmoja wetu anatakiwa kama raia, na kutokana na imani wananchi walio nayo kwetu, kuheshimu, kuzingatia na kutetea Katiba; kutokana na kiapo tulichokula, kila mmoja wetu anastahili kushuhudia imani halisi na utiifu kwa watu na Jamhuri ya Kenya na kutimiza majukumu yetu kwa uaminifu na uadilifu. Haya ni majukumu tuliyokabidhiwa kikatiba. Hiki ni kiapo cha ofisi tulichoapa mbele ya Mungu na raia wenzetu.

Waheshimiwa Wabunge,

Serikali yangu inatazamia kushirikiana na mabunge yote mawili kutekeleza ajenda yetu. Natazamia kuungwa mkono na mabunge yote mawili.

Hata ingawa huenda tukatofautiana mara kwa mara, tunaweza fanya hivyo katika mazingira ya kuheshimiana na kuafikiana. Twapaswa kuwa na maoni yanayotofautiana pasipo kuwa maadui. Kwa moyo huo, naahidi kwamba Serikali yangu itashirikiana na mabunge yote na pande zote za wabunge katika kazi ya kutekeleza ajenda ya kitaifa na kulibadilisha taifa hili. Jukumu la upinzani wenye msisimuko ni muhimu katika utekelezaji majukumu ya mabunge yote mawili. Nakubali na kuheshimu jukumu hilo na natazamia wabunge wote kuitaka Serikali kuwajibika.

Katiba yetu inadhamiria Serikali yenye maafisa wakuu wachache na waadilifu, sio tu katika kupunguza idadi ya Wizara bali kubuni mfumo mpya wa Serikali yote na kubadilisha jinsi iravyofanya kazi.

Tutalainisha mashirika ya Serikali kukomesha utatanishi na uharibifu kutokana na utekelezaji majukumu sawa na kubuni Serikali ambayo inastahili kwa karne ya 21.

Waheshimiwa Wabunge,

Ulimwengu bado unakabiliwa na matatizo magumu ya kiuchumi, huku yakizidishwa na mfumuko wa masoko katika

mataifa ya Ulaya Magharibi na ongezeko la gharama kat Mashariki. Hata hivyo, hapa barani Afrika uchumi w unaendelea kukua huku idadi ya vijana wetu walioelim ikichipuka ulimwenguni. Kenya inaendelea kwa njia nzuri lak bado haijafaulu.

Huku sekta zetu za kifedha na Teknolojia ya Habari Mawasiliano zikijithibiti, sekta zetu za kilimo, utengene bidhaa na uchukuzi ambazo zapaswa kuwa kichocheo ka biashara ya kuuza bidhaa katika mataifa ya nje hazitekele wajibu wao ipasavyo.

Kama taifa, bado tunakabiliwa na changamoto za uk duni, viwango vikubwa vya ukosefu wa ajira na umas uliosambaa.

Lengo la Serikali yangu ni kuifanya Kenya kuwa nch mapato ya kiwango cha kadri katika kizazi hiki. Hii inamaan kuafikia na kudumisha ukuaji wa zaidi ya aslimia ki Viwango vya ukuaji ambavyo, tukiwa viongozi k vitaboresha maisha ya Wakenya; Wakenya wenye ujuzi ku kazi zinazostahili na kukomesha umaskini.

Ukuaji huu utatimizwa iwapo tutazingatia ujumui maongozi sawa na kuwa imara na kwa kujikakamua.

Lazima tutoe kipau mbele kwa usimamizi bora wa fedh umma, hasa kupunguza ujira. Leo hii, matumizi ya mara mara serikalini yameafikia kiwango ambacho itakuwa vig kudumisha huku ikitumia raslimali zilizokusudiwa maendeleo. Lazima tuwajibikie ujira wa umma. Kwa m katika kipindi cha wakati huu cha matumizi ya pesa za Se ajira wa umma umekadiriwa kuwa shilingi bilioni 458. huu ambao ni wa takribani zaidi ya aslimia 12 ya pato letu la jumla, ni wa juu zaidi kuliko viwango vinavyokut kimataifa vya aslimia saba na unatumia karibu nusu ya m yanayokusanywa na Serikali. Hali hii haitawezi

kudumishwa na ni hatari kubwa katika ufadhili wa miradi muhimu ya maendeleo na inaweza kuathiri mno mafarajio ya kiuchumi ya nchi hii.

Nguzo zote za Serikali lazima ziwe kielelezo na kuongoza katika kupunguza ujira wa umma. Lengo letu kama Serikali na bunge lapaswa kuwa upunguzaji wa gharama ya maisha na kuiwezesha Kenya kujimudu kwa ushindani zaidi na hivyo kuongeza nafasi huku pia tukiimarisha viwango vya maisha. Bila shaka hatua hii ndiyo itakayozingatiwa na Serikali yangu.

Tunahitaji kuanzisha mabadiliko ya ustawi wa kiviwanda nchini mwetu. Katika kipindi cha miaka michache ijayo, lazima tuongeze thamani ya mazao yetu na kutengeneza bidhaa zilizokamilika hapa nchini Kenya ambazo tunazitumia kwa wingi katika nyumba na katika biashara zetu.

Lazima tuanzishe kituo cha huduma bora za utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa bidhaa, ukishughulikia uchukuzi, barabara, reli, uchukuzi wa majini, mabomba ya mafuta na maji, bandari, uhifadhi na kawi.

Lazima tuekeze na kuendesha kilimo cha kisasa kwa kuzindua takribani ekari milioni moja mpya za ardhi ili kuendesha kilimo cha unyunyizaji maji mashamba kwa lengo la kukomesha uhaba wa chakula.

Lazima tuimarisha ukuaji wetu kwa kuuza katika masoko ya nje bidhaa za aina mbali mbali, kuongeza thamani na kutengeneza bidhaa mpya na kufungua masoko mapya.

Lazima tuzibe mapengo katika utaratibu wa ukusanyaji wa ushuru na kuimarisha ukusanyaji wa ushuru.

Lazima tupate thamani ya pesa zetu kutokana na utaratibu wa uuzaji na ununuzi wa bidhaa na huduma za Serikali ili tupate thamani kile tunachogharamia kutokana na fedha za umma.

Lazima tubuni mazingira yanayochochea uvumbuzi, uekezaji na ukuaji.

Lazima tupunguze gharama ya bidhaa zinazotumiwa n wananchi wa kawaida, ikiwemo chakula, nyumba, kawi n uchukuzi.

Lazima tuimarisha zaidi uhusiano wetu na washirika wetu w kandaa hii ili kuimarisha ukuaji wa uchumi, nafasi za kazi n masoko.

Lazima tuekeze katika raslimali ya mtaji wetu muhimu, wat wetu na kutoa kile Katiba yetu inataka—ulinzi wa kijamii kw kila Mkenya.

Lengo letu muhimu ni kugeuza uchumi wetu ili bidha tunazouza katika masoko ya ulimwengu ziweze kujimudu katik mataifa ya ulimwengu na kuimarisha ukuaji unaohitajika kubur ajira kwa vijana wetu na kuwakwamua ndugu na dada zet milioni kumi kutoka kwa umaskini ifikapo mwaka wa 2017.


Waheshimiwa Wabunge,

Tunatazamia kuwa na Kenya ambapo kila raia ako hur kujiimarisha awezavyo. Kenya ambapo kila mmoja anawez kutimiza uwezo wake bila kujali anakotoka, mazingir aliyozaliwa au jamii anakotoka.

Hii ndiyo sababu Serikali yangu itafanya kazi kwa kuzingati Nguzo tisa Muhimu.

Nguzo ya kwanza ni uwazi. Tutabuni Serikali ya uaminifu n uwazi, huku kukiwa na huduma za umma ambazo ni wazi na z uwajibikaji kwa watu wanaozitumia huku tukishirikiana n kaunti kutimiza ahadi ya ugatuzi. Tutashirikiana na idara y mahakama kuharakisha na kuthibiti marekebisho ambay yanaendelea kuhakikisha kupatikana kwa haki kwa Wakeny wote na kuimarisha jamii ambapo kila mtu anafurahia ulin: sawa wa sheria. Tutaimarisha utaratibu wa kukabiliana r uhalifu ili kuimarisha utawala wa sheria.

Nitachukua hatua ya haraka kukomesha ufisadi. Ufisa unaifanya nchi yetu kutovutia kama kituo cha uekezaji. Unazu



utoaji wa huduma muhimu zinazohitajika, kuvuruga uadilifu na maadili ya umma.

Naamini mamlaka yanatumika kwa njia nzuri zaidi yakiwa karibu na wananchi. Kwa muda mrefu sasa, maamuzi mengi yameshindiliwa mikononi mwa wachache jijini Nairobi. Utekelezaji ugatuzi ni muhimu kwa maono ya Serikali yangu kwa Kenya—si chaguo, ni jukumu la kikatiba, tunaloshiriki sote. Utaratibu umewekwa wa kutatua matatizo madogo madogo ya usimamizi kwani Serikali yangu imejitolea kutekeleza kikamilifu ugatuzi.

Ili kuthibiti manufaa ya haki na uhuru wa kibinafsi na kuimarisha uwazi na uwajibikaji, pia tutaimarisha kuwepo kwa mashirika ya kijamii ya kusisimua na kuyawezesha kupata raslimali za umma huku pia tukichukua hatua za kisheria kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika kazi zao.

Tutatetea haki za Wakenya wote, kuhifadhi na kuzitetea sio tu kupitia uongozi bora na kuheshimu utawala wa sheria bali pia kwa kutoa haki ya kujithibiti kijamii. Tutapanua utaratibu wa mashirika ya malipo ya uzeeni ili raia wetu wote waweze kuwa na maisha ya heshima katika uzee.

Serikali yetu imejitolea kuhakikisha raia wetu wanaishi, kufanya kazi na kuabudu katika amani. Mwaka jana, tulipeleka vikosi vyetu vya ulinzi nchini Somalia ili kukabiliana na kundi la kigaidi ambalo halikujali thamani ya maisha ya watu wala kuheshimu sheria.

Kwa kufanya hivyo, tuliidhihirishia raia wetu na ulimwengu kwamba tutakabiliana vilivyo na vitisho vya nje kwa raia wetu. Hata hivyo, vitisho vya usalama wa ndani bado vipo. Lazima tutakabiliana vilivyo na wale watakaotishia amani nchini kwa azima na moyo huo huo wa kujitolea kulinda raia wetu. Serikali yangu itaimarisha usalama katika mipaka yetu na kuimarisha uwiano wa polisi kwa raia kote nchini kwa kufikia kiwango cha Umoja wa Mataifa cha polisi mmoja kwa raia 450.

Bunge hili lazima lichukue hatua kwa hatua kuimarisha huduma yetu ya polisi. Lazima tuwajibikie hadhi ya kila mwanamume na mwanamke anayehatarisha maisha yake kuhudumia wananchi na taifa wakilinda maisha yetu na mal yetu. Kutokana na hali hii, tutatoa vifaa kwa kila kitengo cha polisi ili kuimarisha uadilifu na kuhakikisha vinashughuliki kwa dharura visa vyovyote vya uhalifu, hatua hii itajumuisha kufanya kazi kuhakikisha maslahi yao yanalindwa.

Nguzo nyingine tutakayozingatia ni ubunifu wa ajira. Aslimi 40 ya idadi yetu kwa wakati huu haina kazi. Miongoni mw vijana wetu ukosefu wa kazi ni wa juu sana kufikia aslimi 70. Kwa muda mrefu, raslimali hii ya kitaifa haijapewa umuhim unaohitajika na muda na uwezo wa vijana wetu umepotezwa kupitia unywaji pombe na utumizi wa dawa za kulevya. Lazim tushirikiane kuchukua hatua za kutumia muda na vipawa vy vijana wetu kukuza uchumi wetu. Serikali yangu itathibiti i kushirikisha hazina za kibiashara kwa vijana na wanawake kuhakikisha hazina hizi zinapatikana kwa urahisi kwa raia wa katika maeneo ya uwakilishi bunge kupitia utaratibu sawa na u wa hazina za ustawi wa maeneo bunge.

Kulingana na maongozi yetu ya kulainisha Serika tutaunganisha mashirika yanayoitangaza Kenya katika nyar zote za uchumi na kubuni shirika moja lenye uwezo, ujuzi mthabiti wa kuwakilisha na kuitangaza nchi yetu katika mata ya ng'ambo ili kuvutia biashara, uekezaji na utalii kutoka k ulimwenguni. Balozi zetu pia lazima zitumike kutangaza Ken katika mataifa zinazotuwakilisha na hivyo kuziunganisha m kwa moja na huduma hii ya kuitangaza nchi yetu.

Huku tukiwa na labda mojawapo wa vituo bora vya kit ulimwenguni, lazima tuongeze mchango wa sekta hiyo kwa p letu la jumla, kuongeza uekezaji katika muundo msingi wa uwezo na utangazaji. Lengo letu ni kuongeza maradufu viwar vya utalii katika nchi yetu na kufikia watalii milioni tatu ifika mwaka wa 2017.

Tukiwa viongozi tuliojitolea kubadilisha uchumi wa Kenya, lazima tuimarisha uekezaji katika viwanda vinavyochipuka. Serikali yangu itaimarisha sekta ya michezo na ya burudani, ikibuni Mpango wa Kitaifa wa Bahati Nasibu ambao utaimarisha sekta hizo. Vile vile, tutatafuta kwa kushauriana na serikali za kaunti, kujenga viwanja vya michezo katika miji mitano mikubwa nchini.

Wakenya ambao wametambulika kimataifa na kuteuliwa kupokea tuzo za kimataifa wamedhihirisha kwamba kwa kukeza katika sekta za usanii na burudani sio tu tutakuwa tukibuni ajira bali pia tutaimarisha utalii na utamaduni wetu kote ulimwenguni. Hivyo basi, tutatunga sheria kuongeza hadi aslimia sitini ya vipindi vinavyotayarishiwa nchini kutoka kiwango cha wakati huu cha aslimia arubaini ya vipindi vinavyopeperushwa hewani kupitia runinga za humu nchini.

Lazima tutimize Ruwaza ya Maendeleo ifikapo mwaka wa 2030 na kuendelea kuthibiti muundo msingi wetu wa kitaifa, barabara, reli, ujenzi wa nyumba, bandari, shule na hospitali.

Kupitia miradi kama vile Mradi wa Ujenzi wa Ushoroba wa Uchukuzi wa kutoka Bandari ya Lamu hadi nchini Sudan Kusini na Ethiopia—LAPPSET, tutaendesha ustawi wa kiuchumi, kubuni ajira na kuimarisha uhusiano na washirika wetu wa kanda hii.

Hasa taifa letu linahitaji kwa dharura nyumba mpya, tunahitaji kujenga nyumba alfu 250 kila mwaka lakini kwa wakati huu tunajenga nyumba alfu 50 kwa mwaka. Kuhusu uchukuzi, tunahitaji muundo msingi wa ushirikishi wa uchukuzi wa idadi ya watu wengi katika miji yetu na katika mwendo mrefu wa kutunganisha na jirani zetu mbali na kuimarisha barabara za humu nchini ili wananchi wetu waweze kusafiri nchini kwa njia huru. Hata hivyo, ili kuafikia haya tunahitaji kuchukua hatua ya kuongeza mtaji ulioko nchini kwa uekezaji

wa muundo msingi na kuvutia uekezaji wa moja kwa moja kigeni.

Lengo kuu la Serikali lapaswa kuwa utoaji wa huduma kwa wananchi na wala sio tu umiliki na usimamizi wa mali. Hivyo basi, lengo langu ni kuafikia uadilifu na ustadi wa Serikali yangu katika utoaji wa huduma.

Serikali hii itahakikisha kuwepo kwa chakula cha kutos kwa kuwekeza na kuifanya sekta yetu ya kilimo kuwa ya kisa Kupita kuimarishwa kwa ufadhili, unyunyizaji maji mashamba utafiti na ustawi na kurejeshwa kwa huduma za nyanja tutawawezesha wakulima kuacha kilimo cha kawaida kuingilia kilimo cha kibiashara.

Tutaunga mkono Tume ya Kitaifa ya Ardhi na kufadhili ugawaji wa ardhi na utoaji wa hati za umiliki wa ardhi kuwasaidia katika juhudi zao za kumiliki ardhi kama njia moja ya uzalishaji na kuimarisha kujitosheleza kwa chakula.

Serikali hii imejitolea kuhakikisha hali ya juu zaidi ya afya Sera yetu inanuia kuhakikisha Wakenya wote wameafikia viwango vya afya vyenye vifaa na wahudumu wa afya wenye ujuzi motisha mbali na kuimarisha utaratibu wa kuunga mkono kupanua huduma ya afya na usafi bora. Kwa kufanya kazi serikali za kaunti, tutatimiza kujitolea kwetu kutoa huduma maalumu ya afya ya msingi kwa Wakenya wote kufikia mwaka 2020, tukianza na watoto, walemavu, wanawake wajaawazite wanaonyonyesha.

Waheshimiwa Wabunge,

Serikali yangu itaangazia elimu. Sote tunafahamu kwamba elimu na ajira zinahusiana. Tuko katika ulimwengu wa kiuchumi unaozingatia ufahamu na teknolojia. Serikali yangu inatimiza kupendekeza maongozi ambayo yatatoa nafasi ya kuongeza idadi ya taasisi za teknolojia katika kila kaunti na kukomaa mtindo wa wakati huu wa kubadilisha vyuo vya kadri na kutoa vyuo vikuu.

Serikali yangu imejitolea kutimiza ahadi ya patakilishi bila malipo kwa watoto wa darasa la kwanza kuanzia mwaka ujao. Wengine wamesema kwamba mpango huo ni kujitakia makuu—nami nasema kwamba hatuwezi kuacha mmoja wa watoto wetu bila vifaa vinavyowawezesha kushindana katika nyakati hizi za kidijitali. Ndiyo, lengo letu ni kuu, lakini kiwango cha lengo letu ndicho tu kinachotosha kukabiliana na inayokabili changamoto taifa letu. Hivyo basi, natoa wito kwa mabunge yote mawili kushirikiana nami kuhakikisha kwamba patakilishi tutakazotoa siku za usoni zitaundwa hapa nchini.

Nguzo yetu ya nane ni kueneza huduma za kimsingi kama vile maji na stima kwa kila mkenya. Tutaongeza, mwaka baada ya mwaka, tutaongeza huduma ya maji safi kwa idadi ya wanainchi zaidi na kudumisha utoaji wa nguvu za umeme hadi tufikie lengo letu la kutoa maji na stima kwa wakenya wote.

Kuimarisha utoaji wa maji safi ni muhimu kwa malengo ya maongozi yetu, kutasaidia kuzindua ardhi zaidi kwa ukulima, kutaimarisha afya ya raia wetu, kutasaidia kutoa usalama hasa katika eneo la Kenya Kaskazini kwa kukomesha chanzo cha mizozo ya mara kwa mara na kuhifadhi na kuimarisha viumbemazingira.

Kenya imekuwa ikikumbwa na ukame na mafuriko ya mara kwa mara, kila mwaka tunakabiliwa na janga la ukame au mafuriko. Msururu huu unaathiri sana sio tu uzalishaji wa chakula bali pia muundo misingi wetu na uchumi kwa jumla. Tumeziagiza wizara husika kuratibu mfumo wa kujenga mabwawa na mabenesi ya kuhifadhi maji kwa wingi. Mashirika mbali mbali ya serikali yatawaajiri maelfu ya vijana kuanza ujenzi huo mara moja. Tuna vifaa, ujuzi, watu na tutatimiza jukumu hili.

Argentina, ambalo ni taifa lenye mapato ya kadri na lenye idadi sawa ya watu kama Kenya linatoa kiasi cha nguvu za umeme gigawati 24, huku Kenya ikitoa kiasi cha nguvu za

umeme gigawati 1.5. Kawi huendesha uchumi na hivyo b tutaimarisha uekezaji katika nyanja mpya za utoaji nguvu umeme kama vile utoaji nguvu za umeme kwa kutumia miali jua, upepo na mvuke wa ardhi mbali na kutumia mafuta, g na makaa ya moto.

Sekta ya kawi sharti iwekwe huru na kufunguliwa kwa vian vingine vya uekezaji ili tuweze kuimarisha utoaji wa nguvu umeme, kusambaza mfumo wetu wa usambazaji, kuimaris utoaji wa mara kwa mara na wa kiwango cha juu na k gharama ya chini cha nguvu za umeme kwa raia wa Kenya.

Serikali yangu itazingatia jukumu la Kenya itakalotekele katika ulimwengu wenye mabadiliko. Hali ya uhusiano wa tayari inaendelea kubadilika. Tunaimarisha ushirikiano wetu majirani wetu katika kandaa hii. Tunafungamana na ndugu dada wa Afrika katika kuleta amani na uthabiti kote katika b hili. Tunatumia fursa inayochipuka nyakati hizi kuendes ulimwengu na kuiweka Kenya na Afrika katika kiini cha uchu wa ulimwengu. Serikali yangu itaendelea na utaratibu huu k kuhakikisha tunaacha utaratibu wa diplomasia ya kawaida kuanza mawasiliano ya kidiplomasia yanayozingatia masl yetu ya kiuchumi.

Waheshimiwa Wabunge,

Masaa ya bunge hili yameanza rasmi. Chini ya miaka mita kuanzia sasa tutakuwa tunatathminiwa kulingana na ji tulivyoshughulikia masuala yanayokabili nchi hii.

Leo hii, nafafanua ajenda kuu ya utungaji sheria kwa kik hiki cha bunge. Ajenda hii ina Miswaada na Maongozi amb ningeenda yashughulikiwe. Masuala haya ni pamoja na ah tülizotoa na marekebisho ambayo Wakenya walipigia kura.

Kwanza kabisa, Serikali yangu imejitolea kuharakis ukamilishaji wa shughuli za utekelezaji Katiba. Sehemu ya ta ya Katiba inahitaji kwamba sheria zilizosalia zitungwe kabla

tarehe 27 mwezi Agosti mwaka huu. Hivyo basi, nitawasilisha bungeni Mswaada ya:

Kuthibiti haki za raia na kulinda uhuru wa vyombo vya habari;

Kuunga mkono serikali za kaunti;

Kuwawezesha wananchi kushiriki vilivyo katika maamuzi ya kaunti na ya kitaifa;

Kurekebisha ufadhili wa kampeini; na

Kuhakikisha usawa wa kijinsia na wa mchangamano wetu katika mabunge ya kaunti.

Vile vile, nitapendekeza Mswaada wa Ugawaji wa Mapato na Mswaada wa Utengaji wa Mapato ya Kaunti ambayo kulingana na Katiba lazima iidhinishwe ifikapo tarehe 30, Mwezi wa Aprili. Nalihimiza Bunge kuchukua hatua ya dharura katika kushughulikia masuala haya ili tuweze kutimiza majukumu yetu kikatiba.

Mwishowe, kama kujitolea kwangu kutekeleza Katiba, tutaendelea kukadiria utungaji sheria kuhakikisha uzingativu wa Katiba. Tutachukua hatua za haraka kushauriana na mashirika husika yaliyobuniwa kikatiba, wizara husika na idara za Serikali husika kutayarisha mapendekezo ya kuleta uwiano wa maandishi na moyo wa Katiba.

Marekebisho haya yatajumuisha utungaji sheria na marekebisho kuhusu:

Huduma ya Polisi kwa Taifa.

Ushirikishi wa Kitaifa wa Serikali.

Serikali za Kaunti na Ugatuzi.

Usimamizi wa Vifaa vya Matibabu.

Usimamizi wa Elimu.

Kuna mengi ya kufanya katika utekelezaji Katiba. Najivunia kuwahi kuwasilisha kwa wapigaji kura manifesto yenye ufafanuzi, ulinganifu na thabiti kuwahi kutolewa katika historia ya Kenya. Manifesto hiyo imeidhinishwa na Wakenya na nanuia kutimiza ahadi hizo.

Hivyo basi, Serikali itachukua hatua kupendekeza ajenda yetu ya kutunga sheria kulingana na ahadi zilizotolewa katika manifesto ya Jubilee. Nitapendekeza hatua za kulinda familia na kuimarisha kiwango cha maisha bora ya Wakenya.

Vilevile Serikali yangu itatafuta kuthibiti haki na uhuru ambao ni nguzo ya jamii yenye demokrasia halisi kwa kupendekeza kupatikana kwa Mswaada wa Habari na Mswaada wa Kuhifadhi Takwimu.

Serikali hii ni ya wakenya wote iwapo unaishi hapa nyumbani au ng'ambo. Tunatambua mchango wa wale wanaoishi ng'ambi kwa uchumi wa nchi yetu lakini zaidi ya haya yote ni Wanakenya. Hivyo basi, tutachukua hatua za kuwashirikish vilivyo katika maisha ya umma.


Nitachukua hatua madhubuti kuimarisha maendeleo na uwezo wetu kwa ukuaji hasa serikali yangu itachukua hatu zifuatazo:

Kuimarisha na kuthibiti sekta ya Utalii;

Kukadiria na kurekebisha Kifungo cha Sheria ya Ununuzi na Uuzaji wa Bidhaa na Huduma za Umma ili kuanzisha utaratibu wa kisheria kwa Serikali kuwajibika kununua bidhaa na hudu kutoka Kenya na kubuni viwango kwa vijana na wanawake;

Kujumuisha hazina za biashara kwa vijana na wanawake na kubuni hazina mpya yenye uwezo mkubwa ambayo itato huduma zake katika sehemu za uwakilishi bunge;

Kuimarisha na kusimamia sekta ya madini na uchimb madini;





Kuimarisha, kupanua na kuifanya sekta ya kilimo kuwa ya kisasa na kujitosheleza kwa chakula.

Kukadiria sheria zinazohusu makampuni na mashirika mengine ili kuimarisha mazingira ya kibiashara, kupunguza urasimu na kutoa mfumo wa kuaminika wa usimamizi wa biashara; na

Kushirikisha Wakenya wanaoishi ng'ambo kwa masuala ya umma nchini.

Sisi ni wasimamizi wa mazingira yetu, tukiaminika kusimamia ulimwengu huu kwa vizazi vijavyo vya Wakenya. Tunawajibika kuhifadhi mbuga zetu za wanyama pori na mandhari yetu. Hii ndiyo sababu napendekeza sheria za kuimarisha uhifadhi wa mazingira yetu. Miswaada hii inajumuisha:

Mabadiliko katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira yetu.

Kuimarisha na kupanua usimamizi na uhifadhi wa maji.

Kuimarisha upanuzi na usimamizi wa sekta za kawi na mafuta ya petroli.

Kurekebisha usimamizi wa uchimbaji madini na utumizi wa rasilmali ili kuwashirikisha Wakenya wengi zaidi katika sekta hiyo.

Kuchukua hatua za dharura kushughulikia hatari zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Kuhifadhi mbuga za wanyama pori na mazingira yetu.

Ijapokuwa, nchi yetu imeshuhudia maendeleo makubwa katika miaka kumi iliyopita katika muundo msingi wa kitaifa, ni Wakenya wachache ambao wamepata manufaa katika maisha yao ya kila siku. Sasa ni wakati wa Wakenya wote kushiriki katika manufaa yanayotokana na matunda ya ufanisi wetu. Hivyo basi, miswaada ifuatayo nitawasilisha ili:

Kuimarisha ubora na kupatikana kwa elimu.

Kupanua na kuimarisha huduma za afya za kimsingi wanawake wajawazito na watoto.

Kukuza na kupanua sekta za michezo, usanii na burudai kubuni mfumo wa bahati nasibu ya kitaifa.

Waheshimiwa Wabunge,

Serikali yangu imejitolea kutoa suluhisho kwa masual ardhi ili ardhi iweze kubainika kuwa mojawapo wa vinavyochangia uzalishaji miongoni mwa vingi. Tutapende Miswaada kushughulikia:

Kufurushwa na kupewa makaazi kwa wakimbizi wa ndai maskwata.

Usimamizi na Ugawaji wa Ardhi ya Kijamii.

Kukodisha na Kusimamia Mali ya Umma.

Nyanja nyingine ambapo tutapendekeza Miswaada kujadi ni pamoja na:

Msatakabali wa Mashirika ya Serikali.

Kuimarisha huduma za kushughulikia vifo vya ghafla

Kudhibiti sekta ya Huduma za Usalama wa Kibinafsi.

Waheshimiwa Wabunge,

Kazi yetu inaanza saa hii, katika muda wa siku 100 zi tutatimiza yafuatayo;

Tutatoa fedha ambazo tayari zimetengwa kununua madaw vifaa kwa vituo vya afya na zahanati za umma;

Tutafutilia mbali malipo yanayotozwa kwa matibabu k zahanati na vituo vya afya ya umma;

Tutafutilia mbali malipo yanayotozwa wanav wanaojifungua katika hospitali za umma;

Tutawasilisha miswaada ya kupitishwa na bunge kuhakikisha hakuna mtoto anafukuzwa shule au chuo mafunzo hadi atakapotimiza umri wa miaka kumi na minane

Tutabuni mfumo wa kuhakikisha kwamba kila mtoto anayejiunga na darasa la kwanza mwaka ujao anapewa patakilishi; na

Tutabuni mfumo kwa vijana na wanawake kupata mikopo bila masharti yoyote katika sehemu za mashinani.

Waheshimiwa Wabunge,

Iwapo tutatekeleza hatua nilizofafanua leo, nina imani kwamba tutawasaidia watoto wetu na familia zetu; kutukuza matumaini ya waanzilishi wetu na kuthibiti hatima ya Kenya.

Hivyo basi, nawahimiza wabunge wote kujiandaa kufanya kazi iliyo mbele yetu.

Nawakaribisha na kuwahimiza raia wote kuchukua nafasi yao katika utaratibu wa utungaji sheria kama mawakala wa uwajibikaji.

Sawa na Katiba yetu, mamlaka yote ni ya wananchi wa Kenya na hivyo basi nasema Wakenya wenzangu hii ni Serikali yenu. Tukishirikiana, kuwa wakakamavu katika majadiliano na mashauriano yetu basi nina imani kwamba hakuna kinachoweza kutuzuia kuafikia chochote kile.

Hebu muwe thabiti katika matumaini, waaminifu kwa viapo vyenu, msivurugwe na maslahi ya kibinafsi; kutatizwa na changamoto, kutatanishwa na ufanisi na imara katika utoaji huduma.

Hebu muwe washirikishi wa amani mahala kuna uhasama, usalama kunako hofu, umoja kunako utengano na ufanisi kunako ukosefu, hadi maono ya taifa moja, lenye demokrasia na huru yatakapoafikiwa kulingana na Katiba yetu na ari ya taifa letu.

Mungu awabariki raia wa Jamhuri hii na Mungu abariki na kuongoza bunge hili la kumi na moja mnapofuatilia malengo haya muhimu niliyofafanua.

**SPEECH BY HIS EXCELLENCY HON. UHURU  
KENYATTA, C.G.H., PRESIDENT AND COMMANDER  
IN-CHIEF OF THE DEFENCE FORCES OF THE  
REPUBLIC OF KENYA DURING THE STATE  
OPENING OF THE 11TH PARLIAMENT,  
TUESDAY, 16TH APRIL, 2013**

HONOURABLE SPEAKER OF THE SENATE;  
HONOURABLE SPEAKER OF THE NATIONAL ASSEMBLY;  
SENATORS;  
HONOURABLE MEMBERS OF PARLIAMENT;

It is a great honour to address this opening session of Parliament combining both Houses. I congratulate Honourable Members on your election and nomination to both the Senate and National Assembly.

My congratulations also go to the Speakers of the Senate and National Assembly together with their respective deputies on their elections, the leaders of the majority party and minority party as well as their respective deputies on being elected to their positions. I want to especially congratulate the large number of women in both Houses—an indication of Kenya's commitment to achieving gender parity and equity. I commend the last Parliament for the passage of numerous Bills and for meeting constitutional deadlines. I wish all Honourable Members the best as you steer the legislative and policy agenda of this august House over the next 5 years.

We all participated in an electoral process in which we campaigned in different counties and constituencies; contended for different seats and campaigning as members of different parties and coalitions. Today, we come together with a common purpose—that of promoting the welfare of Kenyans, protecting the rights of Kenyans and giving voice to the many and diverse interests of our people. We are here, not for ourselves, but as representatives of the people.

